JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

SHULE YA SEKONDARI KIPAUMBELE,
S.L.P 331,
NACHINGWEA.
TAREHE………………………………

KUMB.NA.AI/KIP/SS/VOL1/…………
NDUGU………………………………………………………..........

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI KIPAUMBELE MWAKA 2021**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kufanya vizuri mtihani wako wa darasa la saba. Nakujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Kipaumbele.

Shule ya sekondari Kipaumbele ipo katika wilaya ya Nachingwea Tarafa ya Nambambo Kata ya Nangowe, shule ipo umbali wa kilometa mbili (2km) kutoka Nachingwea Mjini.

Shule hii ni ya kutwa na ni ya Mchanganyiko wa Wasichana na Wavulana. Shule haina mabweni hivyo Mwanafunzi anatakiwa kulala nyumbani. Ikiwa mwanafunzi anatoka mbali, atalazimika kupanga chunba maeneo ya karibu na shule ili kumwezesha Mwanafunzi kuwahi kufika shule.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ili uzishughulikie na uje nazo bila kukosa siku ambayo mwanafunzi ataripoti shuleni.

1. Fomu namba moja (01) ya kupimwa na Mganga Mkuu Mkoa/Wilaya/Kituo cha afya (isijazwe bila mwanafunzi kupimwa).
2. Fomu namba mbili (02) yenye orodha ya mahitaji muhimu ya shule
3. Fomu namba tatu (03) ni fomu ya sheria na kanuni za shule.
4. Fomu namba nne (04) ni ya ahadi ya mwanafunzi na mzazi /mlezi.

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** kumbuka kuwa Mwanafunzi hatapokelewa endapo atashindwa kuripoti ndani ya wiki ya kwanza ya kufungua shule.

Nakutakia masomo mema, na karibu sana katika shule ya Sekondari Kipaumbele.

………………………………………………
MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY

KIPAUMBELE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 331,
NACHINGWEA.
DATE………………………..

REF: NO…………………
THE MEDICAL OFFICER
……………………………………………
……………………………………………
…………………………………………….

**RE:** REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS…………………………………............................................................

The heading above is concerned.

Please examine the health of the above named student and give us a report regarding his/her suitability for secondary school studies.

1. Student full name……………………………………………………………………………….
2. Blood……………………………………………………………………………………………………
3. Stool…………………………………………………………………………………………………….
4. T.B. test…………………………………………………………………………………………….
5. Syphilis test………………………………………………………………………………………….
6. Urine examination……………………………………………………………………………
7. Eye test………………………………………………………………………………………………
8. Chest…………………………………………………………………………………………………
9. Ears……………………………………………………………………………………………………….
10. Spleen……………………………………………………………………………………………………….
11. Abdomen………………………………………………………………………………………………
12. Pregnancy (Girls only) ……………………………………………………………………………

I certify that above named student is suitable/unsuitable for secondary school studies.

If unsuitable please give reasons.
………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………………………………………………………………..

Name of Medical Officer…………………………………………………………
Signature of Medical Officer…………………………………………………………

Date……………………………………………………………………………………………
Official Stamp……………………………………………………………………………….

**MAHITAJI MUHIMU YA SHULE**

1. (i) **SARE ZA SHULE**
    a) Suruali ndefu mbili (02) nyeusi kwa wavulana zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo. Jinsi staili hazitakiwi kabisa. Sketi mbili kwa wasichana zilizoshonwa kwa unadhifu bila madoido au mitindo, sketi ziwe ndefu kupita magoti na zenye marinda ya wastanii yasiwe madogo sana au mapana sana. Linda box haitakiwi kabisa ( sketi fupi hazitakubalika kabisa).
    b) Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi na yenye kola shingoni ( wavulana na wasichana)
    c) Hijabu nyeupe ndefu inayovuka kiuno kwa Waislam tu wanaohitaji pamoja na na sketi za shule ndefu na sio suruali.
    d) Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili (2), viatu vyenye visigino virefu au viatu vya kupanda havitakiwi.
    e) Soksi nyeusi jozi mbili (02) sio za rangi nyingine au mchanganyiko.

(ii) SARE ZA MICHEZO

sare za michezo ni rangi yz blue kwa wavulana na wasichana. jezi ya timu ya taifa itatumika kama sare ya michezo ya shule. hakikisha inakuwa na bukta yake

2. **VIFAA VYA KUJIFUNZIA**
    a) Daftari zisizo pungua kumi na tano (15)
    b) Karamu (pen), penseli na rula ndefu ya sentimeta 30.
    c) Mkebe (mathematical set)
    d) Kamusi (Dictionary)

3. **CHAKULA CHA WANAFUNZI**
    a) Mboga kilo kumi (10)
    b) Mahindi yaliyo kobolewa kilo 40
    c) Gharama ya kusagia na kulipa wapishi Tsh 14,000/=

    **michango yote iliyotajwa hapo juu ni michango ya mwaka mzima**

    **N.B:** michango inatakiwa itolewe yote siku mwanafunzi anaripoti shuleni ikiwa kamilifu au nusu ya kila mchango.

4. Mwanafunzi anatakiwa kuja na **RIMU** mbili (**02)** za **A4** siku anayokuja kuripoti shule.

5. Mwanafunzi awe amejiunga na mfuko wa afya ya jamii (C.H.F) au mfuko wowote wa bima ya afya unaotambulika na serikali.

6. Aje na jembe au fyekeo (kwanja).

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchin na Ofisi yaWaziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shule.

    a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wot, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
    b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
    c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
    d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
    e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
    f) Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa.
    g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wota kutunza mali za umma.

2. Makossa yanafuata yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

    a) Wizi
    b) Uasherati
    c) Ubakaji
    d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadharika
    e) Kupigana au kupiga
    f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
    g) Kuoa au kuolewa
    h) Kutoa mimba
    i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
    j) Kukataa adhabu kwa makusudi
    k) Kuwa na simu ya mkononi.

## AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

1. AHADI YA MZAZI/MLEZI

   Mimi………………………………………… Mzazi/Mlezi wa ………………………………. Nakubaliana na taratibu, kanuni na sheria za shule na pia niko tayari kufuata maelekezo mengine yatakayotolewa na shule hii.

   Saini………………………………
   Tarehe…………………………….

2. AHADI YA MWANAFUNZI

   Mimi…………………………………………ambaye nimechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari kipaumbele mwaka…………………… nakubaliana na taratibu, sheria na kanuni za shule na niko tayari kuzifuata.

   Saini…………………………………
   Tarehe……………………………….